
# LUGHA NA FASIHI
## katika Mshikamano wa Kitaifa na Uwiano Barani Afrika



**WAHARIRI**

John Kobia
Mosol Kandagor
Leonard Chacha Mwita

# LUGHA NA FASIHI KATIKA MSHIKAMANO WA KITAIFA NA UWIANO BARANI AFRIKA

**WAHARIRI**
John Kobia
Mosol Kandagor
Leonard Chacha Mwita

MOI UNIVERSITY
PRESS

Moi University Press, Moi University, Eldoret

© Idara ya Kiswahili na Lugha Nyingine za Kiafrika,
Chuo Kikuu cha Moi

Kimechapishwa 2019

ISBN: 978-9966-133-55-7

Kimetoleshwa na:
Utafiti Foundation
Outspan, Off Eldoret-Nakuru Road.
P. O. Box 884 – 30100. Eldoret. Kenya.
Tel: +254 722 313 515
Website: www.utafitifoundation.com

# SURA YA ISHIRINI NA SABA

## Nafasi ya Mitandao ya Kijamii katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu

Carren Nyandiba
*Chuo Kikuu cha Rongo*

### Utangulizi

Katika miaka ya hivi karibuni, elimu katika vyuo vikuu imeshuhudia mabadiliko yanayotokana na maendeleo ya jamii. Hii ni kwa sababu hali ya ufunzaji katika vyuo vikuu sasa ni tofauti na ilivyokuwa miaka kumi na zaidi iliyopita. Mabadiliko katika vyuo vikuu yameshuhudiwa katika nyanja zote, ikiwemo ufundishaji. Baadhi ya mabadiliko ambayo yamekumba ufundishaji katika vyuo vikuu yametokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo, hali inayofanya madarasa kuwa na wanafunzi wengi. Aidha, vyuo vimejikuta havina wahadhiri wa kutosheleza mahitaji yao. Katika idara nyingi vyuoni, kuna uhaba wa wahadhiri hivi kwamba wale wachache waliopo hulazimika kufundisha vipindi vingi, na vilevile idara hizo hulazimika kutafuta huduma za wahadhiri wa muda (Onana na wenzake, 2014). Vilevile, vyuo vimejikuta vikilazimika kuanzisha kozi na programu kwa wanafunzi wenye mahitaji anuwai. Mojawapo ya kikundi cha wanafunzi wenye mahitaji ya kipekee ni wanafunzi wanaofanya kazi na kusoma kwa wakati huohuo. Wanafunzi hawa huwa na vipindi jioni baada ya kazi na wikendi ama wakati wa likizo za shule (kwa wale ambao ni walimu). Ongezeko la idadi ya vyuo nchini, idadi ya wanafunzi na idadi ya programu zinazofundishwa pamwe na ukosefu wa fedha za kuwaajiri wahadhiri wa kutosha kuhudumia wanafunzi katika vyuo vikuu limechangia katika upungufu wa wahadhiri wa kufundisha masomo mbalimbali yakiwemo masomo ya Kiswahili.

Kando na suala la uhaba wa wahadhiri, kuna suala la ukosefu wa miundo msingi ya kutosha. Ripoti zimetolewa kuhusu uhaba wa madarasa ya kufundishia, maktaba, maabara na hata vifaa muhimu vya kufundishia kama vile bao nyeupe na chaki. Uhaba huu wa wahadhiri na miundo msingi ya kutosha umechangia katika kudorora kwa ufundishaji katika vyuo hivyo. Hii ni kwa sababu, wahadhiri wanalazimika kufundisha madarasa ya wanafunzi wengi, huku wanafunzi wengine wakikosa kuhudhuria vipindi kwa sababu ya ukosefu wa mahali pa kuketi wakati wa somo. Hali hii inahitaji jitihada za pamoja za serikali, uongozi wa vyuo na wahadhiri katika kutatua suala hilo na kupata suluhu la kudumu kuhusu ufundishaji. Mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumika katika kutatua tatizo la ufundishaji katika vyuo vikuu ni matumizi ya Tehama. Teferra (2014) anadai kwamba majilio ya Tehama yamekuwa na athari kubwa katika ufundishaji, utafiti na uongozi katika vyuo vikuu vya Afrika. Anaendelea kudai kwamba, maendeleo katika Tehama yamechangia pakubwa katika kuimarisha viwango, kuendeleza programu, kutekeleza majukumu tofauti vyuoni na kupanua mitandao ya ushirikiano baina ya vyuo mbali mbali ulimwenguni. Aidha, katika utafiti, maendeleo katika Tehama yamechangia pakubwa katika kurahisisha na kuimarisha tafiti katika vyuo vya Afrika. Vile vile, Tehama imefungua milango kwa aina nyingi za mitandao ya kijamii kama vile *Facebook, WhatsApp,*

# SURA YA ISHIRINI NA SABA

## Nafasi ya Mitandao ya Kijamii katika Ufundishaji wa Kiswahili katika Vyuo Vikuu

Carren Nyandiba
*Chuo Kikuu cha Rongo*

### Utangulizi

Katika miaka ya hivi karibuni, elimu katika vyuo vikuu imeshuhudia mabadiliko yanayotokana na maendeleo ya jamii. Hii ni kwa sababu hali ya ufunzaji katika vyuo vikuu sasa ni tofauti na ilivyokuwa miaka kumi na zaidi iliyopita. Mabadiliko katika vyuo vikuu yameshuhudiwa katika nyanja zote, ikiwemo ufundishaji. Baadhi ya mabadiliko ambayo yamekumba ufundishaji katika vyuo vikuu yametokana na ongezeko la idadi ya wanafunzi katika vyuo hivyo, hali inayofanya madarasa kuwa na wanafunzi wengi. Aidha, vyuo vimejikuta havina wahadhiri wa kutosheleza mahitaji yao. Katika idara nyingi vyuoni, kuna uhaba wa wahadhiri hivi kwamba wale wachache waliopo hulazimika kufundisha vipindi vingi, na vilevile idara hizo hulazimika kutafuta huduma za wahadhiri wa muda (Onana na wenzake, 2014). Vilevile, vyuo vimejikuta vikilazimika kuanzisha kozi na programu kwa wanafunzi wenye mahitaji anuwai. Mojawapo ya kikundi cha wanafunzi wenye mahitaji ya kipekee ni wanafunzi wanaofanya kazi na kusoma kwa wakati huohuo. Wanafunzi hawa huwa na vipindi jioni baada ya kazi na wikendi ama wakati wa likizo za shule (kwa wale ambao ni walimu). Ongezeko la idadi ya vyuo nchini, idadi ya wanafunzi na idadi ya programu zinazofundishwa pamwe na ukosefu wa fedha za kuwaajiri wahadhiri wa kutosha kuhudumia wanafunzi katika vyuo vikuu limechangia katika upungufu wa wahadhiri wa kufundisha masomo mbalimbali yakiwemo masomo ya Kiswahili.

Kando na suala la uhaba wa wahadhiri, kuna suala la ukosefu wa miundo msingi ya kutosha. Ripoti zimetolewa kuhusu uhaba wa madarasa ya kufundishia, maktaba, maabara na hata vifaa muhimu vya kufundishia kama vile bao nyeupe na chaki. Uhaba huu wa wahadhiri na miundo msingi ya kutosha umechangia katika kudorora kwa ufundishaji katika vyuo hivyo. Hii ni kwa sababu, wahadhiri wanalazimika kufundisha madarasa ya wanafunzi wengi, huku wanafunzi wengine wakikosa kuhudhuria vipindi kwa sababu ya ukosefu wa mahali pa kuketi wakati wa somo. Hali hii inahitaji jitihada za pamoja za serikali, uongozi wa vyuo na wahadhiri katika kutatua suala hilo na kupata suluhu la kudumu kuhusu ufundishaji. Mojawapo ya mbinu zinazoweza kutumika katika kutatua tatizo la ufundishaji katika vyuo vikuu ni matumizi ya Tehama. Teferra (2014) anadai kwamba majilio ya Tehama yamekuwa na athari kubwa katika ufundishaji, utafiti na uongozi katika vyuo vikuu vya Afrika. Anaendelea kudai kwamba, maendeleo katika Tehama yamechangia pakubwa katika kuimarisha viwango, kuendeleza programu, kutekeleza majukumu tofauti vyuoni na kupanua mitandao ya ushirikiano baina ya vyuo mbali mbali ulimwenguni. Aidha, katika utafiti, maendeleo katika Tehama yamechangia pakubwa katika kurahisisha na kuimarisha tafiti katika vyuo vya Afrika. Vile vile, Tehama imefungua milango kwa aina nyingi za mitandao ya kijamii kama vile *Facebook, WhatsApp,*

*Twitter, Telegram, Instagram* na *Linkedln* miongoni mwa mingine ambayo imetumiwa na inaweza kutumiwa katika kuendeleza ufundishaji wa masomo katika vyuo vikuu.

Sura hii inalenga kuchunguza namna mitandao hii ya kijamii inavyotumika katika kufundishia Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya. Lengo kuu la sura hii ni kujibu maswali yafuatayo: Je ni mitandao ipi ya kijamii inayotumika katika kufundisha Kiswahili katika vyuo vikuu nchini Kenya? Matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa Kiswahili yana manufaa gani kwa mwanafunzi na mwalimu? Ni changamoto gani zinazokumba ufundishaji wa Kiswahili kupitia kwa mitandao ya Kijamii? Tunatanguliza kwa kuifasili dhana ya mitandao ya kijamii, kisha unafuata uhakiki wa maandishi yanayohusiana na mada ya utafiti. Mbinu zinazotumika katika kufundisha Kiswahili zinajadiliwa baada ya uhakiki wa maandishi, halafu mbinu za utafiti zinafafanuliwa. Kabla ya kuhitimisha, sura inajadili mitandao ya kijamii inayotumika kufundisha, manufaa ya kufundishia mitandao hiyo na changamoto za ufundishaji kwa mitandao hiyo.

**Dhana ya Mitandao ya Kijamii**

Kulingana na O'Keeffe na Pearson, (2011), mitandao ya kijamii ni mawasiliano yaliyowezeshwa na tarakilishi kupitia kwa mbinu na vyombo mbalimbali. Mawasiliano hayo yanaweza kuwa ya matini andishi, picha au video. Aidha mawasiliano hayo hutegemea mtandao katika kuwaunganisha watu au makundi ya watu walio katika sehemu mbalimbali za ulimwengu. Uwezo wa kuwaunganisha watu waliotawanyika katika maeneo mbalimbali ndiyo hufanya iitwe mitandao ya kijamii. Mitandao ya kijamii inayotumika hivi sasa ni kama vile *Facebook, Twitter, WhatsApp, Linkedln, Messenger, My space, Telegram, Instagram, Viber, You Tube*, na blogu miongoni mwa mitandao mingine.

Moran, Seaman na Tinti-Kane (2011) wanadai kwamba, dhana ya mitandao ya kijamii si dhahiri kwa vile kwa mara ya kwanza, ulimwengu umekumbana na njia ya mawasiliano ambayo si tuli. Kwamba katika umbo lake na yaliyomo, mitandao ya kijamii huundwa na kudhibitiwa na watumizi, inaweza kunyumbuliwa na kwamba ni yenye uwazi na demokrasia kuliko mbinu nyinginezo za mawasiliano. Wanaendelea kudai kwamba mitandao ya kijamii ina uwezo wa kubadili maarifa yanavyopitishwa, kubadilishana na kujadiliana ili kuleta mabadiliko ya kijamii na kilimwengu.

Ni katika muktadha huu ambapo tunachunguza matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa Kiswahili. Kwa mujibu wa utafiti huu, mitandao ya kijamii ni majukwaa yanayopatikana kwa njia ya simu za rununu au tarakilishi ambayo wanafunzi wanayatumia katika mawasiliano ya kibinafsi ama ya kiakademia. Mitandao hiyo ni pamoja na *Whatsapp, Facebook, Twitter, Telegram, Instagram* na *Linkedln.* Uchunguzi huu unatokana na sababu kwamba matumizi ya mitandao hiyo yamekithiri mno, kwa vile wanajamii wengi wakiwemo wanafunzi hutumia muda wao mwingi katika mitandao hiyo. Sura hii inajadili maoni ya wahadhiri na wanafunzi kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu. Hii inatokana na haja ya kuchunguza namna uraibu wa wanafunzi (kutumia muda mwingi katika mitandao) unaweza kugeuzwa na kuzalisha matokeo chanya.

**Uhakiki wa Maandishi**

Tunaishi katika jamii ambayo imetawaliwa na kuendeshwa na Tehama. Teknolojia, hususan matumizi ya simu rununu na tarakilishi yamezaa mitandao ya kijamii, ambayo baadhi yao imetajwa katika sehemu iliyotangulia. Vyuo vikuu havijasazwa katika mfumko huo wa matumizi

ya mitandao ya kijamii. Mitandao hiyo inaathiri masuala mbali mbali katika maisha ya mwanafunzi binafsi na makundi ya wanafunzi chuoni.

Kwa mujibu wa McLoughlin na Lee (2010), sekta ya elimu inashuhudia mabadiliko mengi ya kijamii na ya kimfumo kwa sababu wanafunzi wanaofuzu wanatarajiwa kuwa na uwezo wa kutekeleza kazi katika taaluma anuwai na kuendelea kuongeza maarifa katika hatua mbalimbali za maisha yao ya kitaaluma. Hali hii inahitaji wadau katika elimu kufikiri upya kuhusu ufundishaji. Kunahitajika mbinu za ufundishaji zinazowatambua wanafunzi kama washiriki tendi na wazalishi wa elimu, wala si wapokezi kimya wa elimu. Kwa hivyo, kuna haja ya wahadhiri na wanafunzi kukumbatia mfumo unaowahusisha wanafunzi zaidi kuliko ule unaowachukulia wanafunzi kama wapokezi wa maarifa yaliyozalishwa na wengine. Matumizi ya mitandao ya kijamii ni njia mojawapo ambayo kwayo wanafunzi wanaweza kutumia katika kutafiti na kubadilishana maarifa na elimu miongoni mwao na vile vile kati yao na wahadhiri wao.

Akishadidia hoja ya ushirikishwaji wa wanafunzi katika uzalishaji wa elimu na maarifa, Teferra (2014) anasema kwamba, kwa sababu ya mabadiliko changamano ya kijamii na utandawazi, shule na vyuo huwa na majukumu mawili: kwanza ni kupokea mbinu na mitindo ya ujifunzaji wa wanafunzi, na pili ni kuwabadili wanafunzi na kuwaandaa kutekeleza kazi katika ulimwengu unaoendela kubadilika. Wadau wanapaswa kutekeleza mabadiliko yoyote katika ufundishaji kwa kuchunguza na kuzingatia wanafunzi wenyewe, yaani wanachopendelea, mahitaji yao, tabia zao za kijamii na uteuzi wao wa kiteknolojia. Kwa vile wanafunzi wamedhihirisha kutumia muda wao mwingi kwenye simu na tarakilishi, kuna haja ya kufikiri upya jinsi vifaa hivi vinaweza kutumika katika kufanya mambo yanayowafaidi, kama vile kupata elimu na maarifa. Madai haya ya Teferra yanaoana na lengo kuu la sura hii ambayo ni kujadili matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa Kiswahili katika vyuo vikuu.

O'Keeffe na Pearson (2011) wanadai kwamba, kujumuika katika mitandao ya kijamii kuna manufaa kwa watoto na vijana. Manufaa yake ni kwamba huimarisha mawasiliano yao, maingiliano yao ya kijamii na pia ujuzi wao wa kiteknolojia. Wanaendela kudai kwamba mitandao ya kijamii kama vile *Facebook* na *Myspace* huwapa wanafunzi fursa ya kutagusana na marafiki zao, wanafunzi wenzao na watu wengine wanaoingiliana nao. Kulingana na utafiti walioufanya, vijana na watoto wa Marekani hutumia simu zao kuingia kwenye mitandao hiyo angalao mara kumi kwa siku. Ingawa utafiti wa O'Keeffe na Pearson unatoa picha ya mambo yalivyo nchini Marekani, hali si tofauti kule na hapa nchini Kenya. Vijana wengi nchini Kenya hutumia muda mwingi kuingia mtandaoni (wengine hata hufanya hivyo wakiwa darasani).

Seaman na Tinti-Kane (2013) walifanya utafiti kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji. Kulingana na utafiti wao, wahadhiri wengi (59.2%) wa Marekani walikiri kwamba Teknolojia ya mawasiliano ya kidijitali au mitandao ya kijamii ina uwezo wa kutumika katika kufundisha. Asilimia 78.9 ya wahadhiri Wamarekani walidai kwamba mawasiliano ya kidijitali yameongeza maingiliano/mawasiliano miongoni mwao na wanafunzi wao. Aidha, utafiti huo ulibaini kwamba asilimia kubwa ya wahadhiri katika taaluma za sayansi za kijamii (74%) hutumia mitandao ya kijamii ikilinganishwa na wale walio katika taaluma za Sayansi asilia ambao ni asilimia 64. Mitandao ambayo ni maarufu miongoni mwa wahadhiri wa Marekani ni pamoja na *Facebook*, Blogu, *Wikis* na *LinkedIn*. Hata hivyo, ingawa wahadhiri wengi walikiri kwamba mawasiliano kidijitali yameongeza maingiliano baina yao na wanafunzi, ni idadi tu wastani ya wahadhiri waliokiri kutumia mitandao ya kijamii katika ufundishaji wao. Aidha, wahadhiri wa umri wa kati ya miaka 35 na 54 walidhihirisha matumizi ya juu ya mitandao hiyo ikilinganishwa na wahadhiri wa umri chini ya miaka 35 na wale wa zaidi ya miaka 55.

**Mbinu za Ufundishaji wa Kiswahili**

Ufundishaji wa Kiswahili katika madarasa mengi unafuata mkondo ambao umefuatwa kwa miaka mingi, yaani mihadhara. Mhadhara ni mtindo wa ufundishaji wa jadi ambao umekuwa ukitumika kwa muda mrefu katika katika vyuo vikuu (Tudor, 2006). Mhadhara ni mazungumzo, ni mawasiliano ya njia moja kutoka kwa mhadhiri hadi kwa mwanafunzi. Katika mhadhara, mhadhiri huchukua muda mwingi darasani kuzungumza, huku wanafunzi wakiwa kimya wakisikiliza na kupokea maarifa na ujuzi kutoka kwake (Henning, 2008). Kulingana na Huba na Freed (2000) mhadhara kama mbinu ya kufundishia ni ya kawaida na hutumika sana katika ufundishaji katika vyuo vikuu ingawa si faafu kama zilivyo mbinu nyingine ambazo hazitumiki kwa wingi. Mihadhara huwa ya ana kwa ana ambapo mhadhiri huwa darasani nao wanafunzi huwepo pale darasani wakimsikiliza.

Kama mbinu ya ufundishaji, mhadhara una manufaa yake na pia udhaifu wake hasa katika ufundishaji wa Kiswahili. Miongoni mwa udhaifu wa kutumia mihadhara katika ufundishaji ni kwamba wanafunzi mara nyingi hawapewi muda wa kushiriki katika usakaji wa elimu na maarifa. Hii ina maana kwamba wanafunzi wanakuwa wapokezi tu wa maarifa huku walimu wakiwa ndio wazalishi maarifa. Aina hii ya ufundishaji inamnyima mwanafunzi fursa ya kushiriki kikamilifu katika mchakato mzima wa upataji elimu, na huenda ikawa sababu ya wanafunzi wengi wanaofuzu kutoweza kutekeleza kazi kulingana na matarajio ya waajiri wao.

Mbinu nyingine ambazo zinatumiwa katika ufundishaji wa Kiswahili ni pamoja na mbinu za majadiliano na mawasilisho ya darasani. Mbinu ya mawasilisho huhusu wanafunzi kupewa kazi za makundi ama za kibinafsi ambazo wanatafitia na kisha kufanya mawasilisho darasani. Majadiliano nayo kama mbinu ya kufundisha huhusu wanafunzi kupewa mada hapo kwa hapo ama awali ili kutafitia na kisha majadiliano yanafanywa kwa kuzingatia mada hiyo.

Mbinu hizi zote ni faafu kwani hakuna mbinu moja inayoweza kutengwa na kusemekana kwamba ndiyo bora zaidi kutumika katika ufundishaji kuliko nyingine. Hata hivyo, kutokana na maendeleo ya kiteknolojia, na ikizingatiwa kwamba teknolojia inapaswa kurahisisha maisha ya wanajamii, kuna haja ya kuitumia katika sekta zote, ikiwemo ufundishaji wa Kiswahili. Na hilo hasa ndilo lengo la sura hii, yaani kuonyesha namna teknolojia, kupitia kwa mitandao ya kijamii inaweza kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili.

Sura hii ni zao la utafiti mdogo uliofanywa uliowashirikisha wahadhiri kumi na watano (15) wa Kiswahili na wanafunzi hamsini (50) wa Kiswahili. Utafiti huu uliwashirikisha wahadhiri wa kudumu na wa muda katika chuo Kikuu cha Rongo na wachache kutoka vyuo vingine nchini Kenya. Aidha, uliwashirikisha wanafunzi wanaosomea shahada ya kwanza katika chuo hicho. Ukusanyaji wa data ulifanywa kupitia kwa hojaji kusambazwa kwa wahadhiri na wanafunzi. Hojaji zote zilisambazwa kupitia kwa *WhatsApp* ambao ni mojawapo ya mitandao ya Kijamii. Hojaji zililengaa kujibu maswali ya utafiti yafuatayo: Je, ni mitandao ipi ya kijamii inafahamika na kutumika katika ufundishaji wa Kiswahili? Kunazo faida gani za kutumia mitando ya kijamii katika kufundisha Kiswahili? Ni changamoto zipi zinazokumba ufundishaji wa Kiswahili kupitia kwa mitandao ya kijamii? Matokeo ya utafiti huo mdogo ndiyo yamejadiliwa katika sehemu zinazofuata.

**Mitandao ya Kijamii Inayotumika katika Ufundishaji**

Ufundishaji wa Kiswahili kupitia kwa mitandao ya kijamii unafanywa kwa njia mbalimbali na kwa viwango tofauti. Utafiti uliofanywa ulibaini kwamba mitandao ya kijamii inayofahamika na kutumika na wahadhiri wa Kiswahili ni pamoja na *WhatsApp, Facebook, Twitter, Instagram,*

*LinkedIn, Youtube, Viber, Snapchat, Telegram, Tumblr, WeChat, Skype, Google+* na *blog*. Uchunguzi zaidi ulidhihirisha kwamba mitandao inayotumika zaidi ni *WhatsApp, Facebook na Telegram* ikifuatwa na *LinkedIn*. Wanafunzi nao walisema kwamba wanafahamu na kutumia mitandao ya *WhatsApp, Facebook, Twitter, Instagram, LinkedIn, Youtube, Viber, Snapchat, Telegram, WeChat, Skype,* na *blog*. Mitandao iliyotumika zaidi na wanafunzi ni *WhatsApp, Facebook, Youtube, Viber* na *WeChat*.

Kati ya wahadhiri waliohusishwa kumi, na mmoja (11) walikiri kutumia mitandao hiyo katika kufundisha na pia katika kuwasiliana na wanafunzi na kupitisha jumbe muhimu kwao. Walipoulizwa jinsi wanavyotumia mitandao hiyo katika kufundishia, walisema kwamba hutumia mitandao hiyo katika kufundisha kwa njia mbalimbali. Kwa mujibu wa walimu hawa, mojawapo ya njia za kufundisha kwa mitandao ya kijamii ni kwa kurusha miongozo ya kozi kwa *WhatsApp* na *facebook*. Wahadhiri wanne (4) walisema kwamba wao huweka miongozo katika vikundi vya *WhatsApp* ambavyo vinawajumuisha wanafunzi wote katika darasa hilo. Wahadhiri watano (5) walisema kwamba wao huwatumia miongozo hiyo wawakilishi wa darasa na kuwaomba wawasambazie wenzao miongozo hiyo.

Njia nyingine ya kufundisha kwa mitandao ya kijamii ni kutuma matini muhimu kuhusu kozi kupitia kwa *Whatsapp* na *Facebook*. Wahadhiri watano (5) walikiri kutuma matini muhimu za kozi katika mitandao hiyo. Mbali na matini za kozi, wahadhiri watatu (3) walisema kwamba wao huwatumia wanafunzi marejeleo muhimu ya kozi zao kupitia kwa *WhatsApp*. Mhadhiri mmoja alisema kwamba yeye huwatumia matini na marejeleo ya kozi punde tu anapozipata. Alidai kwamba "Mara nyingi mimi hukutana na marejeleo ama matini ambayo ni muhimu kwa kozi ninayofundisha, na papo kwa hapo ninaipiga picha na kuwatumia mwanafunzi wangu". Ilibainika kwamba mtandao ulio maarufu zaidi katika kutuma miongozo, matini na marejeleo ni ule wa *WhatsApp*, ukifuatwa na *Facebook*.

Wahadhiri wawili (2) walisema kwamba wao hutumia mitandao ya kijamii katika kufundishia kwa kuwatumia wanafunzi viungo muhimu vinavyowaelekeza wanakoweza kupata matini ama marejeleo fulani ya kozi wanayofundisha. Viungo hivyo vinaweza kuwaelekeza kwenye makala katika majarida, vitabu vya mtandaoni ama matini zinazopatikana katika mitandao. Aidha mhadhiri mmoja alidai kwamba amewahi kutuma picha na video fupi zinazohusiana na mada fulani katika kozi anayofundisha kupitia kwa *facebook* na *WhatsApp*.

Kati ya wahadhiri kumi na watano (15) waliohusishwa, mhadhiri mmoja alisema amewahi kutumia blogu katika kufundishia. Mhadhiri huyo alisema kwamba walianzisha blogu ambapo wanafunzi waliweza kuandika makala na kuzituma ili kusomwa na kupata mwitikio kutoka kwa wanafunzi wenzao. Mhadhiri huyo alisema kwamba makala zilizotumwa katika blogu hiyo zilitumwa kwanza kwa mwalimu ambaye aliziharirí na kisha kuzitumwa kwenye ukurasa wa blogu la darasa. Kwa mujibu wa mwalimu huyo, mbinu hiyo iliwachangamsha na kuwafurahisha mno wanafunzi.

Kwa upande wa wanafunzi, arobaini na wawili (42) waliohojiwa walisema kwamba walitumia mitandao ya kijamii katika kujifunza kwa njia anuwai. Wanafunzi ishirini na wanane (28) walisema kwamba wamewahi kupokea miongozo ya kozi mbalimbali kupitia kwa mtandao ya *WhatsApp* waliyotumiwa na walimu wao. Aidha wanafunzi kumi na tisa (19) walikiri kupokea matini za makala mbalimbali kuhusu kozi, ambazo pia walitumiwa na wahadhiri wao au nyingine walisambaziwa na wanafunzi wenzao. Wanafunzi hao walisema kwamba baada ya kupokea miongozo hiyo na matini hizo, wao huzisomea hapo hapo kwa simu badala ya kupakua

na kuzichapisha. Ni wanafunzi watatu (3) waliosema kwamba wao hupakua na kuchapisha makala, ingawa walisema kwamba wao hufanya hivyo tu kwa matini zisizoweza kusomeka kwenye rununu.

Wanafunzi saba (7) walikiri kuwa wao hutumia mitandao ya *WhatsApp* na *Facebook* katika kuwasiliana na wenzao kuhusu mada mbalimbali zinazohusiana na somo. Mawasiliano hayo yaweza kuwa na wanafunzi wenzao wa darasa moja ama wanafunzi wa vyuo vingine ambao wanafanya kozi sawa na wao. Kati ya wanafunzi hamsini (50) walishirikishwa katika utafiti huu, wanafunzi tisa (9) walisema kwamba wanatumia mitandao ya *WhatsApp* katika kufanya mijadala ya kiakademia. Walisema kwamba wameunda vikundi ambamo wanapokuwa na swali la darasa ama la kibinafsi wanalijadili badala ya kukutana ana kwa ana. Aidha wanafunzi watatu (3) walisema kwamba wao hutumia mtandao wa *Facebook* katika masuala ya kiakademia. Walidai kwamba wanapokuwa na swali la darasa, waliliweka kwenye ukurasa wao wa *Facebook* na kuwaomba watu watoe majibu kulihusu swali au mada. Kwa vyovyote vile, matokeo haya ya utafiti yanaonyesha kwamba mitandao ya kijamii iliyo maarufu na inayotumika katika ufundishaji kwa viwango anuwai ni *WhatsApp* na *Facebook*. Utafiti pia ulitaka kujua manufaa ya kutumia mitandao ya kijamii kwa wanafunzi na wahadhiri, na matokeo yake yamejadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Manufaa ya Kutumia Mitandao ya Kijamii katika Ufundishaji**

Kuhusu suala la manufaa ya kutumia mitandao ya kijamii, wahadhiri na wanafunzi wote waliulizwa waeleze manufaa ya kutumia mitandao hiyo katika kufundisha/ ujifunzaji wa Kiswahili. Wahadhiri waliotumia mitandao hiyo walisema kwamba mitandao ilikuwa ni njia ya haraka ya kuwafikia wanafunzi wakati wowote na kuwatumia matini ama ujumbe muhimu kuhusu kozi. Mwalimu mmoja ananukuliwa akisema kwamba; "Wakati mwingine unaweza kupata matini fulani muhimu ambayo unaona kwamba inaweza kuwafaa wanafunzi wako, wakati huo huo unawatumia kwenye mtandao wa *WhatsApp*."

Wahadhiri wawili (2) walisema kwamba inaweza kuwa ni njia mwafaka ya kuwapa wanafunzi kazi ya kushughulikia wakati mhadhiri amekumbwa na dharura fulani na kwa sababu hiyo hawezi kufika darasani kabisa ama achelewe kufika . Katika hali hiyo, badala ya wanafunzi kukosa kipindi kabisa ama kumsubiri mhadhiri bila kufanya chochote cha maana, mhadhiri anaweza kuwatumia swali na wanafunzi wakaendelea kulijadili pale darasani wakimsubiri afike ama awatumie matini ambazo wanaweza kuzisoma badala ya kukosa kipindi .

Kwa upande wao, baadhi ya wanafunzi walisema kwamba mitandao ya kijamii ni njia mwafaka kwao kuwasiliana na wahadhiri, wanafunzi na wataalam wengine kuhusu masuala mbalimbali yanayohusiana na kozi. Walisema kwamba mitandao ya kijamii ina uwezo wa kuwaunganisha na wahadhiri hata na wanafunzi wenzao wakati wowote bila kuwataka wakutane ana kwa ana. Kwa njia hiyo, mwanafunzi akiwa na swali kuhusu kozi yake anaweza kuwasiliana na mwanafuzi mwenzake ama mhadhiri na swali hilo likajibiwa.

Wanafunzi pia walisema kwamba matumizi ya mitandao ya kijamii kuna manufaa kwa vile wao hawapendi kuhudhuria vipindi vya ana kwa ana. Wawili walidai (2) kwamba ingekuwa vyema iwapo baadhi ya vipindi vya darasani vingeondolewa na wawe na vipindi vya mtandaoni ambapo mhadhiri anawaongoza katika kujadili mada fulani na kila mmoja wao akichangia kwa kutoa maoni ama kuuliza maswali. Wanafunzi hao waliona kwamba uwezekano wa kuwa na vipindi vya mtandaoni upo na kwamba ni mbinu nzuri ya kufundisha. Aidha, utafiti ulilenga kubaini

changamoto zilizoko katika kutumia mitandao ya kijamii kufundishia na matokeo yake yamejadiliwa katika sehemu inayofuata.

**Changamoto za Kutumia Mitandao ya Kijamii katika Ufundishaji**

Ingawa mitandao ya kijamii ina manufaa yake katika ufundishaji wa Kiswahili, utafiti huu uligundua kwamba matumizi yake yanakumbwa na changamoto mbalimbali. Changamoto ya kwanza na ambayo ni ya msingi mno ni kwamba baadhi ya wanafunzi hawana simu zilizo na uwezo wa kuingia mtandaoni almaarufu *Smartphones*, kwa hivyo watakosa mengi iwapo hiyo ndiyo itakayokuwa njia pekee ya kupata habari fulani kuhusu kozi ama mafunzo ya aina yoyote yatolewayo kwa njia hii. Ni jambo lisilopingika kwamba baadhi ya wanafunzi wanatoka katika jamii masikini na wana changamoto ya kulipa hata karo yao. Kwa hali hiyo, wanafunzi kama hao wanakuwa na ugumu wa kupata hela za kununua simu hizo zenye uwezo wa kupokea mtandao maanake hata simu zenyewe ni za gharama ya juu.

Wengi wa wanafunzi walilalamika kuhusu ukosefu wa data ya kuwawezesha kupokea mtandao ili kupata habari zilizotumwa kule. Mfumo wa mitando nchini Kenya unategemea mteja wa mtandao husika kununua data ambayo inamuwezesha kupokea mtandao kwenye simu yake. Wengi wa wanafunzi walisema kwamba wao hutumia mtandao unaopatikana wakiwa katika maeneo mahususi chuoni. Hii ina maana kwamba wanapokuwa mbali na maeneo hayo na hasa nyakati za usiku na wikendi, hawawezi kupokea mtandao huo na kwa hivyo hawawezi kutuma wala kupokea jumbe kupitia kwa mitandao ya kijamii. Baadhi ya wanafunzi walisema kwamba wanapopokea video na matini kubwa ambazo zinahitaji data nyingi, wao huzifuta bila ya kuzipakua kwa kuchelea kutumia data nyingi.

Kwa upande wa wahadhiri, utafiti huu uligundua kwamba kuna wahadhiri wachache walioona mitandao kama njia ya kutuma jumbe za kibinafsi na wala si njia mwafaka ya kutumika katika kufundishia. Maoni haya yanadhihirisha kwamba mielekeo ya wahadhiri kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii katika kufundishia ni hasi. Maoni haya yanaona na maoni ya Seaman na Tinti-Kane (2013) waliosema kwamba wahadhiri wengi Marekani hawakuchukulia mitandao kama njia mwafaka ya kutumika katika kufundishia.

Aidha, baadhi ya wahadhiri walisema kwamba kuna changamoto ya mtandao kusuasua wakati wanapotaka kutuma ujumbe kupitia kwa mitandao ya kijamii. Hali ya udhabiti wa mitandao inayotumika inategemea mambo kama vile, ni kampuni gani inayotoa huduma hizo, mtumizi wa mtandao huo yuko katika sehemu gani ya nchi na kadhalika. Kwa hivyo. Mhadhiri anaweza kutaka kutuma ujumbe fulani kwa wanafunzi lakini ukakosa kufika wakati ule anapotaka kwa sababu ya mtandao kutokuwa dhabiti.

**Hitimisho**

Sura hii imedhihirisha kwamba, japo si kwa viwango vikubwa, kuna ufundishaji unaofanywa kupitia kwa mitandao ya kijamii. Imeonyesha pia kwamba, wanafunzi na wahadhiri wachache wanafurahia matumizi ya mitandao hiyo katika kufundishia Kiswahili na kwamba wanaona kuwa una manufaa. Ulimwengu tunaoishi unasonga kwa kasi mno hivi kwamba mabadiliko yanazidi kushuhudiwa katika kila sekta. Ili kusonga na wakati, kuna haja ya kuanza kufanya mabadiliko yanayoenda na hali ya mambo ya wakati tunamoishi, huku tukijiandaa kwa mabadiliko ya baadaye. Mbinu mojawapo ya kudhihirisha kwamba tumekumbatia mabadiliko ya wakati ni kutumia mitandao ya kijamii katika ufundishaji. Katika kufanya hivyo, tutakuwa tunatumia uraibu wa wanafunzi (mitandao ya kijamii) katika kuzalisha matunda mazuri (elimu)

Kuna haja ya wahadhiri pamoja na wadau wengine katika elimu hasa ya vyuo vikuu kufikiria upya kuhusu mbinu za kufundisha zinazoweza kuwasisimua na kuwajumuisha wanafunzi wanaoishi katika kipindi hiki ambapo teknolojia inatawala maisha ya jamii. Ukweli ni kwamba, kupitia kwa mitandao ya kijamii, vipindi ambavyo hupita kwa vile mhadhiri amekosa kufika vitapungua kwani mhadhiri atatumia mitandao anuwai ya kijamii kuwafikia wanafunzi wake akiwa popote. Kuna haja ya wadau wote kubadili mielekeo yao kuhusu matumizi ya mitandao ya kijamii katika ufundishaji (kwa kuangazia faida zake badala ya dosari zake). Ulimwengu unasonga kwa kasi mno, na maendeleo yya kiteknolojia hayawezi kukwepwa, ni vyema kusonga na wakati kwa kutumia mbinu mpya katika ufundishaji wa Kiswahili

## Marejeleo


Henning, J. E. (2008). *The art of discussion based teaching: opening up conversation in the classroom.* Newyork: Routledge.

Huba, M. E., & Jann, F. E. (2000). Learner Centred Assessment on College Campuses: Shifting the focus from teaching to learning. *College Journal of Research Practice* 74:759-766. Kindle edition.

Mcloughlin, C., na Lee, M. J. W. (2010). Personalised and Self regulated Learning in Web 2.0 era: Internatinal Exemplers of Innovative Pedagogy Using Social Software. *Australasia Journal of Educational Technology.* 26(1) 28-43.

Moran, M, Seaman, J., na Tinti-Kane, H. (2011). *Teaching, Learning and Sharing: How Today's Higher Education Faculty Use Social Media.* Boston, Pearsons Learning solutions.

O'Keeffe, G. S., na Clarke-Pearson, K. (2011). "Clinical Report- The Impact of social Media on Children, Adolescents and Families." *American Academy of Fediatrics.*

Onana, C. A na wenzake (wh). (2014). *Tuning Africa and Harmonisation of Higher Education: The African Experience.* University of Deusto: Tuning Project.

Teferra, D. (2014). The African Higher Education Landscape: Setting the Scene. Katika Onana, C. A na wenzake (wh). *Tuning Africa and Harmonisation of Higher Education: The African Experience.* University of Deusto: Tuning Project.

Seaman, J., na Tinti-Kane, H. (2013). *Social Media for Teaching and Learning.* Boston, Pearsons Learning solutions.

Tudor, I. (2006). *Trends in higher Education language policy in Europe: The case of English as a Language of Instruction.* Paper presented at the ECORE conference challenges in multilingual societies. June 9-10. Brussels- Belgium.